# Dunia ya Ughaibuni: Usawiri wa Mfalme Sulemani katika Fantasia ya Adili na Nduguze ya Shaaban Robert

**Ahmad Kipacha[1] na Hadija Jilala[2]**
[1]Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela
[2]Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
*[1]ahkipacha@gmail.com*
*[2]dijaah@yahoo.com or hadija.jilala@out.ac.tz*
*[2]OCDIC: 0009-0002-8927-7657*

***Ikisiri***
*Shaaban Robert amepewa sifa na hata kukosolewa juu ya utunzi wa baadhi ya riwaya zake za utanzu wa kifantasia kuwa zina mwelekeo wa kukwepa ukweli na kutia chumvi, zinasifa za kukiuka uhalisia na huwaaminisha wasomaji katika mambo yasiyo ya kawaida. Moja ya kazi hiyo ni Adili na Nduguze inayoelezewa kuwa imechanganya 'jusura na fantasia'. Ni riwaya inayochukuliwa kuwa inakiuka kaida au mviringo wa maisha ya ulimwengu halisi. Hata hivyo sifa za riwaya kama hizo, kupitia mkabala wa uhalisiafifi (surrealism) wa Andre Breton, ni kazi zinazochukuliwa kuwa zina uthubutu, zinazompa mwandishi uhuru wa kujieleza bila kujali mipaka ya tajriba zilizozoeleka katika jamii yake. Hivyo, makala hii inachunguza usawiri wa Mfalme Suleimani katika fantasia ya Adili na Nduguze. Lengo la makala hii ni kubainisha fikra za ughaibu katika jamii ya Waswahili kupitia kisa cha Mfalme Suleiman na kubainisha athari ya mitholojia za kidini katika Uandishi wa Robert kupitia kisa cha Mfalme/Nabii Sulemani. Data za makala hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Aidha, nadharia ya uhalisiafifi imetumika katika kuchunguza, kuchambua na kuwasilisha data na matokeo ya utafiti huu. Kwa hiyo, makala hii inachanganua na kujenga hoja kwamba riwaya ya Adili na Nduguze ni kazi ya kifantansia ambayo imechota uajabuajabu kutoka katika hazina ya mitholojia na visasili vya kidini vinavyohusu asili na hatima ya mwanadamu katika jamii ya Waswahili ambapo mipaka baina ya dunia halisi na ile ya kifantasia na wahusika halisi na wale wakifantasia inavunjwa.*

***Maneno makuu:*** *Fantasia, Mfalme Sulemani, Uhalisiafifi, Dunia ya Ughaibuni*

## UTANGULIZI

Shaaban Robert anaifungua riwaya ya *Adili na Nduguze* kwa kutujengea taswira ifuatayo ya mtawala wa nchi ya Ughaibuni:

> Rai, mfalme wa Ughaibuni, alikuwa mfalme wa namna ya peke yake duniani. Alikuwa na tabia iliyohitilafiana kabisa na tabia za watu wengine wa zamani zake. Tabia yake ilijigawa katika theluthi tatu mbalimbali kama rangi ya ngozi ya punda milia. Kwa theluthi ya kwanza alikuwa msuluhifu akapendwa na watu. Kwa theluthi ya pili alifanana na Daudi akaheshimiwa kama mtunzaji mkuu wa wanyama, na kwa theluthi ya tatu alikuwa kama Suleman akatiiwa na majini (1).

Kuna masuala matatu yanayojitokeza katika simulizi la Robert juu ya mhusika mfalme-Rai, kwamba ipo dhana ya uwanda wa 'Ughaibuni' inayofasiriwa katika *Kamusi Kuu ya Kiswahili (2015)* kama 'istilahi yenye asili ya Kiarabu'- inayotokana na neno 'al-ghaib' lenye kumaanisha dunia sambamba isiyoonekana, 'ugenini au mahali kusikojulikana'(uk.1064). Hivyo ughaibuni, nchi ya mfalme Rai, ni dunia nyingine ndani ya dunia ya msingi. Suala la pili ni sifa ya mfalme Rai kufananishwa na Daudi mwenye kumiliki kundi la wanyama. Sifa hii inatugusia mtoto maarufu atokanae na Daudi ambapo kwenye andiko la *Myths and Legends of the Swahili*, Jan Knappert anatutajia 'Sulemani bin Daudi'[1] (1979:58), au Mfalme Sulemani ambaye anapambwa na sifa za uwezo wa kumiliki na 'kutiiwa na majini'. Knappert anamchambua Mfalme Sulemani kwa kina kuwa Waswahili wanaamini juu ya uwezo aliopewa na Mungu (Allah) wa hekima na maarifa, ujuzi wa nyota na lugha za wanyama. Kwa mujibu wa Knappert, Waswahili humwita Sulemani 'Nabii' (4) na kwamba Mfalme Sulemani:

> '*Commanded the spirits. The evil ones he banned to the outer confines of the earth, the good ones were employed to carry him through the skies to wherever he wished to travel, or dig up precious metals for him, and build his palaces'* (5).
>
> (Aliwaamrisha majini. Majini wabaya aliwafungia katika sehemu kando za dunia, wazuru aliwaamrisha kumsafirisha angani popote alipotaka kwenda au kuwaamrisha kumchimbia vito vya thamani na kumjengea mahekalu)

Sifa ya Mfalme Sulemani ya kutiiwa na 'viumbe wasioonekana kama majini' ni sifa anayopambwa nayo mhusika mfalme Rai katika Fantasia ya *Adili na Nduguze* ya Shaaban Robert. Upambaji wa riwaya ya *Adili na Nduguze* na viumbe majini unaendana na imani ya mwandishi Robert juu ya uwepo sambamba wa viumbe kama malaika, pepo, jehanamu na majini

[1] Angalia sura al-Naml katika Korani juzuu ya 27 aya 15 ambapo sifa za ufalme na unabii za Daudi na Sulemani zinabainishwa.

katika dunia halisi. Majini wanafikiri, wanakula, wanaoa, wanahasira na wanafuraha. Hata hivyo majini wanasawiriwa kuwa wananguvu zaidi kuliko binadamu (Jilani 2018).

Shaaban Robert kwa mujibu wa Wafula (1989) katika kazi yake ya 'The Use of Allegory In Shaaban Robert's Prose Works,' anatutajia sifa ya Robert kuwa ni 'Muislamu'. Wafula anashadidia juu ya mazingira ya mafunzo ya dini ya Kiislamu aliyoyapata Shaaban Robert na jinsi yanavyoakisiwa katika kazi zake za kisanaa. Mfano wa wazi ni pale katika Utenzi wa Adili, ambapo Robert alimtaka mtoto wake amuabudu 'Mungu, Mfalme na wazazi wake kama chanzo cha mafanikio yake kimaisha' (55). Wafula analiweka wazi suala la itikadi na maadili ya Robert kwa dini ya Kiislamu na kwamba Korani imemwathiri Robert kifikra. Si ajabu kwa Robert kuathirika hivyo. Madumula (2009) anahitimisha kuwa karibu riwaya zote za Shaaban Robert ni mifano ya riwaya za 'kimaadili' (64). Swali tunalojiuliza ni kwa kiasi gani mwandishi kama yeye huathiriwa na itikadi na maadili yanayomzunguka? Na je atahri hiyo ina mchango gani katika utunzi wa kazi zake za sanaa? Hitimisho la Wafula ni kwamba:

> 'Shaaban Robert's concern with these moral concepts in the abstract inspires him to write mainly about Utopian' (59) (Mtazamo wa Shaaban Robert unaojidhihirisha katika dhana za kimaadili umemuathiri kiasi cha kuandika zaidi kazi za kitopia/kifantasia).

Kazi za kitopia au kifantasia ni zipi? Kwa mujibu wa Colin Manlove ni zile zinazojishughulisha na ulimwengu zaidi ya huu wa kawaida, zaidi ya ule unaojulikana, ulimwengu usiojulikana, na zaidi ya ule unaoaminika (1). Manlove anazichukulia tanzu za kifantasia kama bunilizi zinazoibua uajabu wenye vipengele vya dunia na viumbe vinginevyo. Manlove anauchukulia uajabu wa dunia na viumbe kuwa ni kila kinachohesabika kama zaidi ya kile kinachoaminika au kufikirika katika dunia halisi. Manlove anaamini kuwa ni uhalisia usio na upendeleo unajenga fantasia ya kweli kwa sababu "only those who know one world thoroughly can make another with the inner consistency of reality". Ni wale tu wanaoifahamu dunia moja kisawasawa ndiyo wanaweza kuiunda nyengine kiuhakika) (260). Kwa Manlove anaamini kuwa, dunia ya fantasia ambayo mwandishi amekusudia kuijenga haina budi iwe halisia kama ilivyo dunia yetu (12).

Naye Rosemary Jackson anaamini kwamba fantasia haiundi dunia isiyo ya wanaadamu. Hutumia na kuchanganya vipengele vya dunia hii, "in

new relations to produce something strange, unfamiliar and apparently 'new', absolutely 'other' and different" (katika mahusiano mapya ili kuunda kitu cha kigeni, kisicho cha kawaida na kipya, kilicho kingine na tofauti kabisa) (8). Jackson, anabaini zaidi kuwa chimbuko la fantasia zinatokana na visasali vya kale, sanaajaadiya, na hata ngano (4). Tahadhari anayoitoa Jackson, katika kazi yake ni kwamba dhana ya fantasia inatumiwa kiholela kumaanisha kazi za kifasihi zisizojihusisha na uhalisia, 'realms other than the human' (vikoa zaida ya binadamu) (Jackson, 13-14). Wajibu wa kuunda dunia nyingine ni muhimu kufanyika katika kazi za ubunilifu hususani kazi za kifantasia.

Sambamba na mawazo ya Jackson, Ann Swinfen naye anaeleza kuwa fasihi inahitaji kutumia vipengele vitokanavyo na uhalisia, katika dunia tuifahamuyo. Vipengele hivyo vinaweza kupinduliwa ili kumfanya msomaji ataharuke. Na ili kazi ya kifantasia ifanikiwe vipengele vilivyopinduliwa havinabudi viige vile vipengele vya kihalisia.

Kwa upande wa Tzvetan Todorov, mahusiano baina uhalisia au usohalisia katika matini za kifantasia ndio moyo wa fasihi. Kuna mahusiano baina ya uhalisia wa nje kama tunavyoufahamu na uhalisia anaouibua mwandishi wa fantasia. Uhalisia unatawaliwa na 'by laws unknown to us' (kanuni ambazo ni ngeni kwetu) (25). Kwa mantiki ya mawazo ya Manlove, Jackson, Swifen na Todorov, chimbuko la utopia au ufantasia wa kazi za Robert hautokani na ndoto zake mwenyewe bali ni athari itokanayo na anga la fikra za kighaibu za wanajamii yake na yeye ni mwakilishi tu. Anapomtaja mfalme Rai basi kivuli chake ni Mfalme/Nabii Sulemani wa kihalisia. Hivyo dunia ya ughaibu si njozi kwa Robert.

Kwa mujibu wa Richard Wafula, anambainisha Robert kuwa amelelewa katika methali, misemo na simulizi za watu wake. Umahiri na imani yake inajidhihirisha katika sanaa yake (61). Kuna dalili kuwa kimawazo ameathirika na imani yake ya Uislamu hususani jamii, viumbe na suala zima la ughaibu. Sehemu kubwa ya fikra za Robert ni masuala yanayosawiriwa katika Korani na mitholjia inayobainishwa katika kazi ya Jan Knappert ya *Myths and Legends of the Swahili.* Mfano mmojawapo wa kuathiriwa kwa Robert na mitholojia ya kidini ya Kiislamu unabainishwa na Deo Ngonyani pale anapofafanua kuwa Robert alikuwa na mtazamo wa kina wa kidini-'deeply religious outlook' (133). Anatutolea mfano wa jina la kimitholojia la 'Majuju' (Biblical Magog), ambalo amelitumia katika riwaya ya *Kusadikika* kuwa kwa mujibu wa

masimulizi ya Kiislamu siku ya hukumu kiumbe huyo atakula kila kitu mpaka mawe (128). Hivyo uteuzi wake wa majina ya wahusika umekuwa ukiakisi mafundisho ya dini ya Kiislamu kwa mwandishi huyo (135).

Kupitia mitholojia ya Waswahili, kwa mujibu wa Knappert na imani ya dini ya Kiislamu, suala la uwepo wa viumbe visivyoonekana kama majini si fikra za kiutopia au za kindoto. Hivyo, imani ya uwepo wa viumbe visivyoonekana lakini vinaishi na kuvinjari katika dunia halisi na hata dunia isiyoonekana ya ughaibuni ni suala linalotilia shaka hoja ya kuwa kazi za kifantasia hususani za Shaaban Robert zina mwelekeo wa ‘kukwepa ukweli na kutia chumvi’, na zinasifa za kukiuka ‘uhalisia’ na ‘huwaaminisha wasomaji katika mambo yasiyo ya kawaida’. Je, ukweli na utiaji chumvi katika fikra za Mswahili na mitholojia yake kwa ujumla ni upi? Mipaka ya uhalisia ikoje kwa Mswahili kama Shaaban Robert? Na kitendo cha kuwaaminisha wasomaji katika mambo yasiyo ya kawaida kikoje?

Angalizo la Mugyabuso Mulokozi kuwa kuna masimulizi ambayo ‘huaminiwa kuwa kweli tupu na ni sehemu ya visasili vya kidini vinavyohusu asili na hatima ya mwanadamu’ katika jamii fulani fulani, ikiwemo jamii ya Waswahili (230). Na kwamba mara nyingi hadithi kama hizo ‘hutumika kuelezea au kuhalalisha baadhi ya mila na madhehebu ya jamii inayohusika, ni inayohitaji kuangaliwa kwa jicho pevu. Mulokozi anabaini kuwa visasili vya kidini ‘hufafanua na kueleza masuala magumu yanayohusu mwanadamu kama vile asili na hatima ya mwanadamu, asili ya kifo, asili na hatima ya ulimwengu, Mungu, miungu, mizimu na uhusiano wao na wanadamu’ (101). Hapa Mulokozi anatutahadharisha kuwa tuwe macho katika uchanganuzi wa kipi huhesabika kama kweli tupu na kipi kinawekwa katika kapu la kutokuaminika. Simulizi inapokuwa imeegemezwa katika visasili vya kidini, visasili ambavyo vinaakisi ‘mambo yasiyo ya kawaida’ basi kipengele cha kuwaaminisha wasomaji hakina budi kuangaliwa kwa jicho pevu.

Kwa kupitia mtazamo wa André Breton wa uhalisia fifi katika andiko lake la "First Surrealist Manifesto," ambapo huzichukulia kazi za kifantasia au zenye kusawiri matendo yasiyowezekana katika hali halisi hususani sifa zake za mazingira ya kimetafizikia, taswira za kinjozi au mazingira ya ajabuajabu kuwa ni uthubutu. Breton anasisitiza umuhimu wa uotaji ndoto, uhuru wa kukiuka fikara za kihalisia na kuzivinjari dunia nyingine ambapo hakuna kujiwekea mipaka ya kififikra bali kuruhusu kutanua vikoa vya uwezekeno kwa kuhoji kaida zilizozoeleka.

Hivyo, katika makala hii tunaenda mbali kidogo ya fikra za Breton, tunajenga hoja kuwa iwapo mwandishi anaisawiri jamii yenye fikra zisizo na mipaka baina ya dunia halisi na ile ya kighaibu, au kuwajadili wahusika halisi na wale wasioonekana kwa macho, basi kitendo hicho cha uthubutu ni kuakisi hali halisi ya dunia ya mwandishi huyo. Tunajiuliza swali mtambuka, je, kuna haja gani ya kumshutumu mwandishi kuvuka mipaka ya uhalisia iwapo jamii yake inaamini fikra za 'kifantasia' ambazo mwandishi ameamua kuzisawiri? Iwapo mpaka kati ya mitholojia na imani ya kidini ya mwandishi ni mwembamba, na wakati dini ni mfumo wa imani na matendo juu ya kuabudu nguvu za kiungu na ambapo mitholojia ni mkusanyiko wa visaasili, au hadithi za dini fulani au utamaduni katika kuelezea matendo, imani au tukio fulani. Uhusiano wa visasili vinavyohusu watu au vitu vya kufikirika au ambavyo haviwezi kuthibitika au mfumo wa fikira za kale ambao hauna waumini unaweza kusababisha fikra potofu kwamba visasili ni visa vya ubinifu. Hivyo waumini walio wengi hawaafiki hadithi zao zinazoshabihishwa na dini kama visaasili tu.

Kwa hiyo, hoja kwamba mitholojia za kidini zinafifia kutokana na mabadiliko ya kijamii na hususani kutokana na ukuaji wa sayansi na teknolojia kama anavyogusia Thomas Lombardo hazijaweza kushika mizizi katika jamii ya Robert. Imani ya kuwepo kwa dunia mbili tofauti na viumbe vyenye maumbile tofauti si suala la ajabu kwa jamii iliyomzunguka Robert. Ni sehemu ya mitholojia yenye mlengo wa kidini wa jamii ya Waswahili. Hivyo, tuliona kuna haja ya kufanya utafiti kuhusu dunia ya ughaibuni: usawiri wa mfalme sulemani katika fantasia ya *adili na nduguze* ya shaaban Robert. Tatizo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza jinsi Mfalme Suleimani anavyosawiriwa katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi mawili ambayo ni: kubainisha fikra za ughaibu katika jamii ya Waswahili kupitia kisa cha Mfalme Suleiman na kubainisha athari ya mitholojia za kidini katika Uandishi wa Robert kupitia kisa cha Mfalme/Nabii Sulemani. Aidha, utafiti huu uliongozwa na maswali kwamba iwapo kauli ya Robert kuwa 'Rai mfalme wa Ughaibu, alikuwa kama Sulemani akatiiwa na majini (1)' ni kauli inayochota idhibati ya kutoka fikra za kihalisia za jamii ya Waswahili? Hivyo basi, kupitia utafiti huu tutaweza kudhihirisha jinsi usomaji huu wa Mfalme Sulemani katika *Adili na Nduguze* unavyoendeleza maarifa ya kifantansia katika fasihi ya Kiswahili. Makala hii inaonesha jinsi msanii ama mwandishi anavyoweza kutumia ubunifu wake kuwasilisha masuala ya kijamii.

## DUNIA YA UGHAIBU KATIKA FASIHI YA KISWAHILI

Fasihi ya Kiswahili inahuisha na kugongelea misumari fikra za 'kighaibu' kwa wasomaji wake. Kazi ambazo si ngano au za fasihi simulizi zinajipamba na vichwa vya kighaibu na haswa ubainishaji wa uwepo wa mahali au viumbe vya 'kifantasia': '*Mzimu* wa Watu wa Kale' (Abdulla 1958), 'Ndoa ya *Mzimuni'* (Nuru) na Sofia *Mzimuni'* (Habwe 2006); 'Aliyeonja *Pepo'* (Topan), '*Pepo* ya Mabwege' (Mwakyembe 1981), 'Paradiso' (Habwe 2005) na 'Bustani *ya Edeni'* (Mbogo 2002); Kisima cha *Giningi* (Abdulla 1968) na 'Kija chungu cha Mwana wa *Giningi'* (Kitogo 2005). Hapa dhana za 'mzimuni', 'pepo', 'Paradiso, 'Eden' na 'Giningi' ni sehemu zinazogusia fikra za kighaibu. Kwa upande wa viumbe visivyoonekana kimaada tuna "Mashetani" (Hussein 1971) na *Ziraili* na Zirani (Mkufya 1999) na *Zimwi* la Leo (Wamitila 2002).

Kwa upande wa sanaa-jaadiya ya Waswahili hususani misemo na methali nayo haikuacha kurejelea dhana za kighaibu kama vile '*Mungu* si Athumani', *Zimwi*[2] likujualo halikuli likakwisha, '*Kuzimu* hakusemi siri zake', '*Kuzimu* kuna mambo' na 'kila *shetani* na mbuyu wake'. Huwa hatuhoji unjozi au ufantasia pale tunapozitumia dhana hizo za 'kighaibu' katika mazungumzo ya kawaida. Hii inaashiria kuwa matumizi ya dhana hizo za kighaibu zinaakisi fikra za kimithioljia za Kiswahili zilizoshika mashiko katika jamii.

Katika maandishi ya kiethnografia, kihistoria na hata kileksigrafia kuna masimulizi ya fikra za 'kighaibu' za Waswahili. Kazi ya Amour Abdalla Khamis (2008) ya 'Jadi na Utamaduni wa Mswahili wa Zanzibar katika Utamaduni wa Mzanzibari' anasimulia kihalisia masuala yafuatayo:

> Itikadi iliyombaya ni kwa baadhi ya Waswahili kutenda mchezo wa kwanga usiku na kupelekana Giningi. Wanga hujigeuza paka, mbwa na mifano ya wanyama mbalimbali. Uzoefu unaonyesha kuwa baadhi ya maeneo ya kusini Unguja wana tabia ya ubaya kwa kutumia pungu na chui. Eneo la Kaskazini Unguja hadi Pemba kwa tabia ya kufanyiana ubaya kwa kutumia mashetani na vizuu' (15).

Kuna dalili za uhusianishaji wa kile ambacho Amour anatugusia kinachofahamika katika mitholojia ya Kiswahili ya uwepo wa viumbe vingine 'visivyo vya kawaida' kama vile nunda mla watu, shetani, ibilisi, chunusi, popobawa, vibwengo, mazimwi, na mizimu ambao husawiriwa kama sehemu ya maisha halisi kwa mujibu wa imani na itikadi za Waswahili. Imani ya kuwepo kwa viumbe vya kifantasia ni sehemu ya

[2] KKK (1190) kiumbe dhahania anayesemekana kuwa na madhara na hutumika katka uhusika wa hadithi nyingi na ngano

imani za kitamaduni, kosmolojia, na uoni ulimwengu wa Waswahili unaooanisha vipengele vya kiasilia, kiroho na kiungu.

Uchunguzi wa dhana mbalimbali za wahusika na mandhari za 'kighaibu' katika Kiswahili unapewa uzito na uwepo wa tafsiri zake katika *Kamusi Kuu za Kiswahili* (2015). Mfano dhana ya 'mzimu' ni 'neno la asili lenye kumaanisha mahali panapofanyiwa matambiko ambapo aghalabu huwa ni chini ya mti mkubwa au pangoni. Maskani ya watu waliokufa ambapo watu huamini kuwa kwamba wanaweza kwenda kufanya mawasiliano na wazee wao wa zamani kwa haja mbalimbali kama kuomba mvua (769).

**Ufantansia katika Fasihi ya Kiswahili**

Sifa ya ufantasia imegubikwa katika riwaya zipatazo nne za Shaaban Robert, Wahakiki wanazichukulia riwaya za Robert za *Kusadikika*, *Kufikirika*, *Adili na Nduguze* na *Siku ya Watenzi Wote* kuwa ni bunilizi za kifantasia. Kyallo Wamitila anazibainisha 'riwaya hizo kuwa zinasawiri mazingira, mandhari au matukio ambayo yana msingi mkubwa wa njozi au utopia ambapo matukio ya kinjozi huwekwa kwenye msingi wa ulimwengu halisi' na 'hukiuka kaida au mviringo wa maisha ya ulimwengu halisi au ulimwengu wa kijarabati' (118). Wahakiki Wafula na Njogu wao wanazibaini riwaya hizo kuwa zinasifa ya wahusika wa 'kiajabu ajabu', wenye ushujaa, na ni mifano ya riwaya za kilimbwende (59). Mhakiki Saidi Mohamed[3] amezitaja riwaya hizo kuwa ni riwaya zenye 'mwelekeo wa kukwepa ukweli na kutia chumvi' (21). Kwa upande wa Joshua Madumula yeye amezibainisha riwaya zote za Shaaban Robert kuwa ni mifano ya riwaya za kimaadili ambazo zimeandikwa kwa muundo wa kifasihi simulizi (64-65) huku akiungwa mkono na Fikeni Senkoro kuwa riwaya hizo ni zenye kubugikwa na 'sifa za kingano' na hekaya (54). Makala yetu yanailenga riwaya ya *Adili na Nduguze* pekee inayobainishwa na Mugyabuso Mulokozi kuwa ni riwaya yenye kuchanganya 'jusura[4] na fantasia' (246). Mapungufu ya riwaya za kinjozi au kifantasia, kwa mtazamo wa Senkoro ni kule 'kukosekana kwa uthibitisho' hivyo riwaya hizo zinasifa za kukiuka uhalisia na huwaaminisha wasomaji katika mambo yasiyo ya kawaida (99). Hata hivyo Samwel Method[5] anaenda mbali zaidi na kuzibainisha riwaya hizo

[3] Said Ahmed Mohamed 1995 Kunga za Nathari ya Kiswahili: Nairobi: East African Educational Publishers.
[4] Kwa mujibu wa Mulokozi (2017: 246), 'jusura ni masaibu au mikasa yenye kusisimua damu ambayo mtu huweza kukutana nayo wakati wa kutekeleza jambo fulani', mfano Adili anaposafiri na kufika katika mji wa mawe.
[5] Angalia Method Samwel (2015) *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahil*i Dar es Salaam: Meveli Publishers Ltd

kuwa ni riwaya dhidi ya utawala wa kikoloni zilizoandikwa kwa kutumia 'lugha ya picha ya kiwango cha juu sana' (234).

## METHODOLOJIA YA UTAFITI

Makala hii inahusu Dunia ya Ughaibuni: Usawiri wa Mfalme Sulemani katika Fantasia ya *Adili na Nduguze* ya Shaaban Robert. Data za makala hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini wa Fantasia ya *Adili na Nduguze* (2010) iliyoandikwa na Shaaban Roberth. Mtafiti alisoma riwaya hiyo na kisha kukusanya data zinazohusiana na ufantansia wa Adili na nduguze katika fasihi ya Kiswahili ili kukidhi malengo ya utafiti huu. Mtafiti pia alisoma machapisho mengine yanayohusiana na mada hii katika tovuti na kwenye maktaba mbalimbali ambayo kwa ujumla wake yalisaidia kujaziliza data za utafiti huu. Makala hii imetumia mkabala wa kitaamuli katika ukusanyaji, uchambuzi, uwasilishaji na mjadala wa data na matokeo ya utafiti huu. Mkabala wa kitaamuli ni mkabala ambao data zake zinafafanuliwa kwa kutumia maelezo na si takwimu katika kuwasilisha na kujadili data za utafiti. Uwasililishaji wa data, uchambuzi na mjadala wa matokeo ya utafiti huu yanajidhihirisha katika vipengele cha 4.1 na 4.2.

## UWASILISHAJI WA DATA

Kama tulivyoeleza makala hii ililenga kuchunguza usawiri wa Mfalme Suleimani katika fantansia ya *Adili na Nduguze*. Kwa kutumia mbinu za usomaji makini, mtafiti alisoma, kuchambua na kubainisha fikra za ughaibu katika jamii ya Waswahili kupitia kisa cha Mfalme Suleiman na kubainisha athari ya mitholojia za kidini katika Uandishi wa Robert kupitia kisa cha Mfalme/Nabii Sulemani.

### Dunia ya Ughaibu ya Mfalme Rai na Mfalme Sulemani

Utafiti huu ulilenga kuchunguza fikra za ughaibu katika jamii ya Waswahili kupitia kisa cha Mfalme Suleiman. Utafiti huu umebaini kuwa, Shaaban Robert katika *Adili na Nduguze* ameichora ramani ya dunia kwa namna ambayo hazishii katika dunia ya wazi bali inahusisha pia dunia nyinginezo (otherworld) zisizoonekana wazi lakini zenye maumbile na viumbe tofauti kama vile majini, mtu-mnyama. Dunia hizi tofauti zake haziko mbali ingawaje zina mipaka ya *Kufikirika*. Waliopo dunia nyinginezo wanaingalia dunia ya wazi kwa ukaribu mno na wana uwezo wa hali ya juu na nguvu kupita kiasi katika kuyaingilia maisha ya waliopo katika dunia ya wazi. Kwa mfano kuna Rai ambaye ndiyo mfalme wa Ughaibuni na Watawaliwa ambao ndio raia wa ughaibuni. Mwandishi anasema;

*Rai, mfalme wa Ughaibu, alikuwa mfalme wa namna ya peke yake duniani.*

*"……Kutawala suluhu na mapenzi ya wanadamu, utunzaji wa wanyama, na utii juu ya viumbe wasioonekana kama majini hutaka uwezo mkubwa sana. Kmama hivi, fikiri wewe mwenyewe jinsi Rai alivyojipambanua mwenyewe na wafalme wengine".*

Usanifu majengo wa dunia ya ughaibuni unapewa sifa za ziada, sifa za uajabuajabu. Katika mji wa mawe, Adili alipopanda gorofani, alifika 'kulikokuwa na chumba kidogo Mlango wake ulikuwa wazi, kwa hivi aliingia ndani. Huko aliona pazia la Hariri lililotaraziwia kwa vito vya dhahabu, lulu na yakuti linaning'inia mbele yake' (25). Hivyo majengo ya aushi ya kuvutia, makasri ya ajabu, mabarabara yaliyosakafiwa na mitaa iliyopangiliwa, madaraja ya ajabu kwa ujumla usanifu majengo wa ajabu unapewa nafasi kubwa katika bunilifu za 'kifantasia' ili kumpa picha msomaji wa dunia nyengine.

Katika riwaya hizi tunaona mwandishi anavyowachora viumbe vya ughaibuni kwa kuvipamba na sifa za ziada ili kuwatofautisha na viumbe wa dunia halisi. Kwa mfano, mwandishi anatuonesha Adili akikutana na mwanamke mwenye sifa za ziada alipofika katika mji wa mawe. Alikutana na msichana ambaye 'uso wake ulikuwa umetukuka kwa uzuri uliokuwa haumithiliki' (25). Hata mavazi yake hayakuwa ya kawaida kwani 'libasi' yake haina mfano hapa duniani. Msomaji anapokuja kutambulishwa msichana huyo ambaye hana mfano wake katika dunia halisi kuwa ni jini, hashituki kwani sifa za ziada tayari zilishatangulia machoni pake. Hali hii inadhihirisha ufantansia katika ubunizi wa *Adili na Nduguze*.

Hivyo kitendo cha Adili kutembelea mji wa mawe, Ikibali katika kutembelea mji wa Janibu na jumba la liwali katika riwaya ya *Adili na Nduguze* ni maandalizi ya mwandishi ili kumtayarisha msomaji kupokea uajabu na 'ufantasia' anaojengewa kifikra. Kwa vile usanifu majengo wa tanzu za kinjozi ni ujenzi bandia, muundo wake hauna budi kuwa muundo usio wa kawaida. Hivyo, waandishi wa tanzu zenye ufantasia huibua uwezekano wa kuwa na vifaa vya usanifu majengo vinavyowafanya wajifikirishe na kuzichunguza kwa kina njia zao za kukabiliana na ulimwengu.

Usambamba wa walio na nguvu na wasioonekana haupo tu kwa viumbe visemekavyo ni majini, mizimu, mashetani, malaika n.k tukiwachukulia

kuwa viumbe hao ni viumbe wa kisitiari basi picha inabadilika na kutuletea uhalisia wa maisha hapa duniani. Utafiti huu umebaini kuwa, uthubutu wa Robert ni ule wa kuwafanya wasomaji wake waone kuwa kuna mstari mwembamba baina dunia halisi na ile ya ughaibu, na kuna mashirikiano baina ya viumbe wasioonekana na viumbe maada. Kupitia *Adili na Nduguze*, Robert anawabainishia wasomaji kuwa katika dunia ya Waswahili, ufantasia si mbadala wa uhalisia. Bali ufantasia ni mlengo tata unaojidhihirisha katika maisha ya kila siku hapa duniani. Andre Breton anasisitiza umuhimu wa njozi na fikra huria na kuvunja mipaka ya fikra za kimantiki na kuzamia fikra huria ili kuibua mambo yaliyojificha. Hakuna mipaka ya mbali baina ya dunia ya mzimuni na dunia halisi. Hakuna mipaka baina ya viumbe visivyoonekana na vile vinavyoonekana. Hivyo, mkabala wa uhalisafifi unatoa leseni kwa Robert kuvunja fikra za uwepo wa mipaka ya mbali.  Robert anawapa nguvu wasomaji wake kuamini yale yanayohisiwa kuwa hayawezekani kutokea.

Utafiti huu ulibaini kuwa ubunifu wa Robert katika riwaya hii, unaashiria kitendo cha mwandishi kutaka asihukumiwe kwa kuwachora wahusika majini, mizimu, mashetani n.k katika riwaya hiyo. Ni sawa na kusema kuwa kwa vile imani ya Mungu, majini, mizimu na mashetani kwa upande mmoja na imani ya miji ya kighaibu kwa upande wa pili ni mseto wa dunia mbili na aina za viumbe ambavyo vipo duniani kwa sasa. Si ndoto kwa Robert pale anaposimulia yafuatayo:

> Tukufu alimtazama msemaji akasema kwa ukali, "Nini kilichokujusulisha kusema upuzi Mrefu? Kama kwa sababu ya urefu wako ubongo wako umeyeyuka kwa jua, kaa kitako chini ya kivuli cha mizimu yetu utaburudika. Kama umerogwa, Kabwere atawakomesha waliokuroga. Riziki ya wanadamu hutoka mimeani. Kwa sababu hiyo, mimi na kaumu hii twaabudu miti. Funga ulimi wako, bwana. Usipofunga hasira ya mizimu itakuwa juu yako (29).

Hapa Robert anaisawiri dunia yake halisi ya Uswahilini, kuwa kuna imani ya viumbe vya majini, kuna imani ya marogo, na kuna imani ya kuabudu mizimu na nguvu za laana ya mizimu. Mwandishi anadhihirisha hilo kwa kusema;

> “Walakini, juu ya sifa hizo, malkia, mfalme na raia walikuwa waabudu mizimu. Mizimu yao ilikuwa miti. Miti yenyewe ni ile iliyogeuka kuwa mawe ukutani. Kawere, mganga na imamu wa mizimu hiyo alivuta mioyo ya watu wote” (uk. 27).

Hii hali si ufantasia kwa Robert na Waswahili. Unapoamini uwepo wa majini hushtushwi na kitendo cha Mrefu ‘kuzunguka dunia nzima kwa

sekunde moja' (29). Hushtushwi na laana ya watu wa kawaida kugeuzwa manyani, au mawe. Hushtushwi vilevile na viumbe vya dunia ya ughaibu inapowasiliana na kukutana na watu wa dunia halisi.

Hivyo, utafiti huu ulibaini kuwa kitendo cha Robert kutuanishia dunia mbili na viumbe vya aina mbili ni uthubutu wa kutufikirisha na kutupoza wasomaji juu ya kile ambacho kinaelea katika dunia halisi. Bado dunia inahitaji majibu ya kina juu ya uwepo wa mtagusano baina ya dunia na viumbe vya dunia nyingineo. Wasomaji wa riwaya za Robert zenye mkondo wa 'kifantasia' wanawezeshwa na Robert kubaini kanikinzani ya kihalisia ya wanajamii yake. Kwa mujibu wa miongoni mwa wananadharia wa mkondo wa kifantasia, Kathryn Hume anajenga hoja kuwa dhima ya utanzu wa kifantasia ni kule kuonyesha ukinzani dhidi ya kile kifikiriwacho na kinachokubalikwa na wengi kuwa ni uhalisia au uwezekano. Wahakiki walio wengi huitupia lawama utanzu huu wa kifantasia kuwa ni upo tu kama sehemu ya kuukwepa uhalisia na kuacha kusawiri yaliyowazi.

Utafiti huu ulibaini kuwa, kitendo cha Robert cha kuwafanya viumbe wasio wanadamu kama vile majini, manyani, ndege, nyoka, tandu kuwa sehemu ya maisha ya jamii ya Shaaban Robert katika *Adili na Nduguze* huonekana kama ni kitendo cha ukwepaji wa uhalisia. Hebu na tuangalia kiusambamba je, viumbe hivyo visivyohalisia vinatenda matendo yapi? Manyani-wanadamu yaliyolaaniwa, majini-nyoka na tandu, ndege mwokozi, majini mema wanakuwa wahusika muhimu katika riwaya. Viumbe wasio wanadamu wanakinzanishwa na viumbe wanadamu katika dunia mbili tofauti: dunia halisi na dunia nyinginezo. Maisha ya dunia hizi mbili yanalandanishwa. Viumbe hivyo visivyoonekana vyenye nguvu na maajabuajabu wanatumika kurekebisha maisha ya kidunia wakiwa wahusika kutokea dunia nyingine. Dunia nyingine ni makazi yanayokaliwa na viumbe visivyowanadamu au viumbe vinginevyo. Mfalme Sulemani anazifahamu lugha za wanyama, majini, ndege na ana uwezo wa kuamrisha upepo. Hivyo anautawala wa ngazi ya juu ya viumbe na mazingira yake. Katika Korani, Mfalme Sulemani anajulikana kama Nabii Sulemani, mwenye vipawa vingi. Viumbe majini wanaingilia maisha ya dunia halisi. Tofauti kubwa kati ya majini na wanadamu ni kile kitendo cha kuonekana na kutokuonekana. Majini na viumbe visivyoonekana wanauwezo wa kutenda matendo ya ajabu ajabu. Kwa mujibu wa David Johnson viumbe hivyo huweza kusaidia kuwafanya watu halisi wajione kwa ufasaha zaidi.

## Athari ya Mitholojia za Kidini katika Uandishi wa Robert

Makala hii ilichunguza athari ya mitholojia za kidini katika riwaya ya *Adili na Nduguze* Uandishi wa Robert kupitia kisa cha Mfalme/Nabii Sulemani. Kwa kutumia mbinu ya usomaji makini tuliweza kubaini jinsi mwandishi alivyoathiriwa na dini ya Kiislamu na Korani katika utunzi wake wa riwaya ya *Adili na Nduguze*. Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kwamba, Shaaban Robert si tu kwamba anatuundia sifa za za Mfalme Rai wa nchi ya ughaibuni huku katika jamii yake kukiwa na fikra na imani ya kuwepo katika dunia halisi ya Robert juu ya fikra ya Nabii/Mfalme Sulemani katika Korani anayesadikika alikuwa akiwatiisha majini na wanyama na hata upepo. Bado Mfalme Rai anapambwa na sifa ya kitendo chake cha kulikagua kundi lake la wanyama na kuona 'karibu mazizi yote katika miliki yake yamekwisha lipa kodi zake ila mazizi ya Janibu' na hivyo akaamuru uchunguzi ufanywe (3). Kitendo hiki kinasawiri kisa cha Mfalme/Nabii Sulemani ndani ya Korani cha Nabii/Mfalme Sulemani kukagua makundi mbalimbali yakiwemo watu, majini, na wanyama na kukuta ndege aina ya 'hudihudi'[6] hayupo katika milki yake hivyo alitaka kujua sababu ya kutokuwepo kwake.
Utafiti huu ulibaini kuwa, katika *Adili na Nduguze* mwandishi anatusawiria viumbe na miji jinsi ilivyogeuzwa mawe huku kukiwepo na kisaasili katika mitholojia za Kidini za mke wa Nabii Luti kugeuka jiwe. Katika Biblia Mwanzo 19.26 mke wa Lut aligeuzwa jiwe la chumvi alipokaidi amri ya kutokugeuka nyuma wakati wa kuangamizwa kwa mji wa Sodoma.

Vile vile utafiti huu uligundua kwamba, ughaibu unajidhihirisha pale ambapo mwandishi anaunda viumbe waliogeuzwa manyani. Kitendo hiki kinajidhihirisha katika Korani ambapo inasimulia uwepo wa viumbe waliogeuzwa manyani kwa kuvunja siku ya Sabato ambapo Sura 2 aya 65 inazungumzia laana waliopewa waumini waliovunja amri ya kutofanya kazi siku ya Sabato, wao wakaamua kuvua samaki na Mungu kuwageuza manyani. Hii inadhihrisha kuwa mwandishi anatumia visa vya Korani kuwasilisha ujumbe katika jamii yake. Matumizi haya yanatudhuhirishia

[6] Katika Korani Nabii Sulemani alibaini kutokuwepo kwa mmoja wa raia zake, ndege aina ya Hudihudi. Alitaka kujua sababu za kutokuwepo kwake. Aliporudi Hudihudi alimletea taarifa za ugunduzi wa uwepo wa mtawala anayeabudu Jua badala ya Allah. Nabii Sulemani alithibitisha maneno ya Hudihudi na akamtaka malkia huyo awache kuabudu masanamu na kumwabudu Mungu na iwapo hatakubaliana naye atamshambulia kivita. Kisa hiki kinabaishwa katika Korani, juzuu ya Al-Naml, 27, aya 20-22.

athari ya Imani ya dini ya mwandishi katika ujenzi wa visa na matukio katika uhalisia wa jamii inayomzunguka.

Lengo la makala hii ni kubainisha fikra za ughaibu katika jamii ya Waswahili kupitia kisa cha Mfalme Suleiman na kubainisha

## HITIMISHO

Makala hii imejadili kuhusu Dunia ya Ughaibuni: Usawiri wa Mfalme Sulemani katika Fantasia ya *Adili na Nduguze* ya Shaaban Robert. Kipindi alichokuwa akiandikia trilojia za Kusadikika, Kufikirika na Adili na Nduguze, Robert na jamii yake alikuwa katika lindi la ukoloni mkongwe, kipindi cha ubaguzi, na unyanyasi wa wazawa na hivyo mwandishi hakuwa na budi ya kupambania hali yake na mustakbali wa wanajamii yake. Tunaweza kujenga hoja kwamba ufantasia unatoa nafasi ya mwandishi kuwa huru kifikra na kuelezea yanayomsibu kibunilifu bila ya hofu ya kutiwa misukosuko na watawala. Makala hii inachanganua na kujenga hoja kwamba baadhi ya kazi hizo za kifantasia, kama ilivyo *Adili na Nduguze*, huchota uajabuajabu kutoka katika hazina ya mitholojia na visasili vya kidini vinavyohusu asili na hatima ya mwanadamu katika jamii ya Waswahili ambapo mipaka baina ya dunia halisi na ile ya kifantasia na wahusika halisi na wale wakifantasia inavunjwa.

## MAREJEO

Anne, D. W. (1983). *Magical Thought in Creative Writing. The Distinctive Roles of Fantasy and Imagination in Fiction.* Stroud: The Thimble Press.

Breton, A. (1969). *The Manifesto of Surrealism*. Trans. Richard Seaver and Helen R. Lane (Michigan: Ann Arbor Paperbacks

David, K. J. (2022) On angels Demons and Ghosts: Is Justified Belief in Spiritual Entities Possible? In *Religions* 13(7) 603).

Irwin, W. R. (1976). *The Game of the Impossible: A Rhetoric of Fantasy*. Urbana; London: University of Illinois Press.

Jan, K. (1979). *Myths and Legends of the Swahili*, Label mounted on t. p.: Humanities
Press, New York

Jilani, T.M. (2018). *Jinn and its Effects on Muslim Society*. *Glob J Arch & Anthropol*.; 6(4): 555694. DOI: 10.19080/ GJAA.2018.06.55569.

Madumula, J. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: nadharia, historia, na misingi ya uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers

Kamusi Kuu ya Kiswahili (2015). Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Karl, M. & Friedrich, E. (1995). *Selected Works of Marx and Engels*. Beijing: Renmin chubanshe.

Knappert, J. (1979). *Myths and Legends of the Swahili.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Kyle, J. D. (2022). On angels Demons and Ghosts: Is Justified Belief in Spiritual Entities Possible? In *Religions* 13(7) 603).

Legere, K & Mkwarihembo, P. (2008) *Hadithi za Benedicta*. Publication Ndanda Peramiho

Lombardo, T (2006). "Ancient Myth, Religion, and Philosophy" in Lombardo, Thomas (2006). *The Evolution of Future Consciousness*. Bloomington, Indiana: Author House,

Madoshi, J. (2015). Folk narratives and the reflection of (utu) humanness in shaaban robert's Adili na Nduguze. *The Belogradchik Journal for Local History, Cultural Heritage and Folk Studies* Volume 6, Number 1, 2015 111-121

Manlove, C. (1975). *Modern Fantasy. Five Studies*. Cambridge: Cambridge University Press.

Risco, A. (1982). *Literatura y Fantasia*. (Madrid: Taurus Ediciones S. A, 1982), p. 133

Ronen, R. (1994). *Possible Worlds in Literary Theory*. Cambridge: Cambridge University Press,

Jackson, R. (1981). *Fantasy. The Literature of Subversion.*London & New York: Routledge.

Topan, F. (1971) *Mfalme Juha*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Swinfen, A. (1984). *In Defence of Fantasy. A Study of the Genre in English and American Literature since 1945.* London: Routledge & Kegan Paul.

Todorov, T. (1970). *The Fantastic in Fiction*. Twentieth Century Studies.

Wafula, R. (1989). 'The Use of Allegory in Shaaban Robert's Prose Works, Master of Arts Thesis. *University of Nairobi*. Nairobi.

Wamitila, W. K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Yusuf Ali, A. The Holy Qur'an Translation and Commentary, Islamic Propagation Centre International, 124 Queen Street, Durban 4001.